

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”

EPIISODE 7: “Promise”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: DAY IN THE CITY

- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Aster (f, 15)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE TWO: DAY AT ASKALE’S HOUSE

- **Askale (f,21)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Samy (m, 6)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE THREE: DAY IN THE CITY

- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Aster (f, 15)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE FOUR: DAY IN THE CITY, AT A GARBAGE CONTAINER

- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Begidu (m, 7)**
- **Street boy (m, 12)**
- **Aster (f, 15)**
- **Narrator (m/f)**

INTRO:

Hamjambo! Karibuni kwenye mchezo wetu wa redio wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Hii ni sehemu ya saba iitwayo “AHADI.” Kumbula Begidu mtoto mdogo wa Kassech ametoweka kwa zaidi ya nyumba. Mara ya mwisho, tulimsikia Aster akisema anajua aliko Begidu. Lakini ni wapi aliko? Kwa habari zaidi, endelea kutusikiliza. Papa Tilahun na Mama Beletu wakiwa pamoja na mjukuu wao Aster wanasubiri teksi kwenda mjini.

SCENE ONE: DAY IN THE CITY

1. SFX: TRAFFIC NOISE (next to busy street)

2. Papa Tilahun: Sasa, unajua kwa hakika mahali penyewe?

3. Aster: Ndiyo, Ninajua.

4. Mama Beletu. **(Hesitant)** Na rafiki yako Semira alikuwa na hakika?

5. Aster: Ninamwamini. Katu hasemi uongo.

6. SFX: CAR APPROACHING

7. Papa Tilahun: **(In a hurry)** Basi, isimamishe hiyo teksi. Tusichelewe sana.

8. Aster: **(Calls)** Teksi! Teksi! **(runs)** Teksi!

9. SFX: CAR BRAKING AND STOPPING

10.NARRATION: Papa Tilahun na Mama Beletu wamempangishia Kassech chumba, kwa hivyo wanamjua vyema Begidu, mwanawe Kassech. Wanataka kumrejsha mtoto wake pasi na kumwambia. Wameamua kutompasha yale mjukuu wao aliyowaambia. Lakini wana taarifa kiasi gani? Huku watu hao watatu wakielekea mjini kutoka kitongojini mwao, Kassech na rafiki yake Askale wanakaa nyumbani kwa Askale. Kassech anashangaa kuona jinsi Samy anavyofanya vizuri kazi ya shule.

SCENE TWO: DAY AT ASKALE’S HOUSE

11. SFX: PAPER IS BEING TURNED

12. Kassech: Naona Samy anaelewa sana somo la herufi.

13. Askale: Naam!

14. Kassech: Mashaallah! Hata maandishi yako yanavutia sana, Samy.

15. Samy: **(Laughs joyfully).**

16. Askale: Unasema nini pale mtu anapokusifu kwa jambo ulilotenda?

17. Samy: Asante sana, Bi Kassech!

18. **Kassech:** Si neno, Samy! Wewe ni mtoto ni mzuri sana!

19. **Askale:** Kila mara mimi huangalia kazi zake za shule na pia huangalia tabia yake.

20. **Samy:** Mama, nimuonyeshe Bi. Kassech michoro yangu?

21. **Askale:** **(Motivating)** Sawa! Ilete hiyo michoro kisha umuonyeshe Kassech.

KW Begin

22. **Kassech:** Naam, nionyeshe. **(He walks away joyfully).**

23. **Askale:** Anapenda sana kuchora.

24. **Kassech:** Loo! Inapendeza sana. **(Regretfully)**
Sikukukaa muda mwingi na mwanangu nakumhimiza kufanya kama hivi. Nilidhani kuwa inatosha kwamba hana njaa wala kiu. Lakini alikuwa na njaa na kiu- ya mapenzi!

25. **Askale:** Lakini unapenda sana. Unahitajika kumwonyesha hayo Begidu.

26. **Kassech:** Lakini vipi, Askale? Sijui nifanye vipi. Ni kiasi wiki mbili tangu alipotoweka wala hakuna mtu ambaye amempata. **(Sobs)** Sijui iwapo nitampata mwanangu akiwa hai **(more sob)**.
27. **Askale:** Itakuwa heri, Kassech. Usiwe na wasiwasi. InshaAllah tutampata hivi karibuni. Nina hakika. **(Samy comes back)**.
28. **Kassech:** Mashaallah! Samy.
29. **Samy:** Michoro yangu hii, Bi Kassech.
30. **SFX: SHUFFLING PAPER**
31. **Kassech:** Loo! Mchoro huu unapendeza sana.
32. **Samy:** Unaupenda?
33. **Kassech:** Naam, ninaupenda.
34. **Samy:** Na mimi pia!

KW END

35. **Askale:** Ebu nione, **(pause)** mashaallah! Wewe ni mchoraji mzuri sana **(Samy laughs joyfully)**.
36. **Kassech:** Tuambie kuhusu wavulana wawili walio kwenya mchoro?
37. **Samy:** Wavulana hao ni marafiki wa dhiti.

38. **Kassech:** Wanafanya nini?
39. **Samy:** **(Proudly)** Wanakumbatiana. Huyu ni mimi na huyu ni Begidu.
40. **Kassech:** **(Sobs).**
41. **Samy:** Ma, mbona analia? Bi Kassech, kwani michoro yangu haikupendezi?
42. **Kassech:** **(Sobbing stops)** Sivyo, sivyo hata, naipenda sana. Inavutia sana! Sikujua kwamba wewe ni mchoraji mzuri kiasi hicho.
43. **Samy:** Ikiwa unapenda michoro yangu, ninaweza kukuchorea pia.
44. **Kassech:** Asante, Samy.
45. **Askale:** Haya mwanangu, Samy, basi nenda chumbani utuchoree picha nyingine. Sawa.
46. **Samy:** Sawa, ma. **(In hurry)** Niende chumbani mwangu na michoro yote hii?
47. **Askale:** Naam! Ichukue.
48. **SFX: SHUFFLING PAPER**
49. **Samy:** **(Joyful)** Sawa ma, nitumie ile rangi nyekundu ulioninunulia jana?

50. **Askale:** Bila shaka, itumie. **(He goes).**
51. **Kassech:** Ajabu! Wewe si kama mimi. Wewe ni mvumilivu kwa kiasi kikubwa!
52. **Askale:** Naam, watoto wanahitaji kuvumiliwa sana!
53. **Kassech:** Ninamtamani sana mwanangu! Ninaahidi, iwapo polisi watampata, nitampenda kwa moyo wangu wote. Na nitafanya mambo mengi mazuri kuliko nilivyofanya hapo awali. Naahidi.
54. **Askale:** Hiyo ni mara ya pili unatoa ahadi.
55. **Kassech:** **(Laughs)** Mara ya tatu hii hapa. NINATOAHADI!
56. **NARRATION:** Wakati Kassech anapotoa ahadi mara ya tatu kwamba atampa malezi mema mwanawe, wenye nyumba na mjukuu wao Aster wameshafika mbali safarini mwao. Wanaposhuka kwenye tekisi jijini, wanashuhudia jambo la kushangaza kando ya barabara.

SCENE THREE: DAY IN THE CAPITAL

57. **SFX: CITY NOISES (traffic, people)**
58. **Aster:** Mungu wangu! Yule pale, si niliwaambia?
59. **Papa Tilahun:** **(Surprise)** Ni yeye kweli?

- 60. Mama Tilahu:** Una maana gani, Papa Tilahun? Yule ni Begidu, mwanawe Kassech.
- 61. Papa Tilahun:** Basi, tunasubiri nini?
- 62. Mama Tilahu:** Hapana, hapana! Subiri, acha tuone anachokifanya pale alipo. Huenda akakimbia pindi akituona.
- 63. Aster:** Naam, afadhali tusebiri kidogo.
- 64. Papa Tilahu:** Kuna watoto wengine anaoandamana nao.
- 65. Mama Tilahu:** Wote wamevaa mararu tena ni wachafu! (**feels a great deal of pity**) Maskini! Kassech yuko wapi amwone mwanawe.
- 66. Papa Tilahu:** Aster, kweli unayosema!
- 67. Aster:** Naam! Semira hajawahi kunidanganya.
- 68. Papa Tilahu:** Huyo ni rafiki mzuri.
- 69. Mama Beletu:** Mbona Semira hakumzungumzia pale alipomuona?
- 70. Aster:** Kusema kweli, alimkaribia lakini akakimbia pindi alipomuona.
- 71. Papa Tilahu:** Maskini, Watizame! Wanakwenda kwenye pipa la taka.

72. Aster: Mungu wangu! Wote wanaingia kwenye pipa la taka!

73. Mama Beletu: Tazama wanachofanya!

74. Papa Tilahun: Sasa twendeni huko waliko! Tuharakisheni!

75. NARRATION: Begidu na watoto wengine wa mitaani wameanza kuchokora pipa la taka wakitafuta chakula. Hili ni jambo la kawaida kote barani Afrika. Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto yaani UNICEF, kuna watoto zaidi ya milioni mia moja wa mitaani kote ulimwenguni; ambapo milioni thelathini miongoni mwao wanapatikana katika bara la Afrika. Kuna sababu kadha wa kadha zinazosababisha watoto hao kuwa mitaani. Baadhi yao hawana makazi kwa sababu ya umaskini, vita au vifo vya wazazi wao kutokana na maradhi ya UKIMWI. Wengine wanatoroka nyumbani mwao kutokana na ulevi na ugomvi wa wazazi wao au pia kutelekezwa kama Begidu alivyotelekezwa.

SCENE FOUR: DAY IN THE CITY, AT A GARBAGE CONTAINER

76. SFX: TRAFFIC NOISES

77. SFX: SEARCH IN RUBBISH

78. Street boy: Nini hicho, ndizi? Ebu nipe mimi, ewe kifupi nyundo!

79. Begidu: Lakini mimi pia sijala kitu tangu asubuhi.

80. **Street boy:** Hayo hayanihusu, hata mimi sijala.
Nimekwambia unipe!
81. **Begidu:** Sikupi hata kidogo, mwenyewe nafa njaa.
(Starts to eat fast)
82. **Street boy:** **(Hits Begidu's head)** Nitakufunza adabu!
83. **SFX: BANG ON HEAD**
84. **Begidu:** Aaagh! **(Cries).**
85. **Papa Tilahun:** **(Approaching)** Acha! Achana naye! Usimpige!
86. **Street boy:** Hayakuhusu! **(He hits Begidu again and runs away)**
87. **SFX: SOMEONE RUNS AWAY**
88. **Begidu:** **(Cries more).**
89. **Mama Beletu:** Amempiga kichwani!
90. **Papa Tilahun:** Subiri! Nimesema, usimame!
91. **Street boy:** **(Laughs from a distance)** Ebu njoo unikamate mzee! Kimbia! Hunishindi hata nikikimbia kwa mguu mmoja. Tayari, moja, mbili, tatu, kimbia, kimbia **(laughs and runs).**
92. **Mama Beletu:** Maskini watoto wa watu!
93. **Aster:** Njoo hapa, Begidu. Nitakushika mkono.

94. **Begidu:** Aster! **(Cries)**.
95. **Aster:** Sawa! Bahati iliyoje kwetu sisi kukupata!
96. **Papa Tilahun:** Mfff! Hapa pahali pananuka si haba!
Tuondokeni hapa. Twende zetu, Begidu.
97. **Mama Beletu:** Uko salama sasa. Tutakurudisha nyumbani.
98. **Begidu:** Hapana. Sitaki kwenda nyumbani mimi.
99. **Aster:** Usijali, twende pamoja.
100. **Papa Tilahun:** Mwanangu, mbona hutaki kwenda nyumbani?
101. **Begidu:** **(Cries)** Mama atanipiga. Ananipiga kila mara.
102. **Mama Beletu:** Hatakupiga tena!
103. **Aster:** Hakuna mtu atakayekupiga tena.
104. **Papa Tilahun:** Mamako anakupenda sana. Anajuta sana kwa vile ambavyo amekuwa akikutendea. Analia kila siku kwa kuwa anakutamani sana wewe mwanawe.
105. **Begidu:** **(Sobs)** Mama.

KW begin

106. **Mama Beletu:** Maskini mtoto wa watu! Sasa turudi nyumbani.

107. **Begidu:** Ninahisi njaa.
108. **Aster:** Bila shaka una njaa. Tutakuandalia chakula kitamu nyumbani!
109. **Mama Beletu:** Ndiyo sababu tumekuja kukufuata. Twende nyumbani sasa.
110. **Begidu.** **(Smiles)** Sawa! Tutakwenda.

KW end

111. **Papa Tilahun:** Tuondokeni sasa.

112. **SFX: THREE PEOPLE FOOTSTEPS**

113. **SFX: ASTERS CELLPHONE RINGS**

114. **Aster:** **(Joyfully)** Naam! Semira!...Ndiyo, tumempata!...Naam, pale pale uliponiambia. ... Ulinifahamisha vizuri mahala ambapo ningempata. **(Excited)** Asante sana, rafiki yangu!...Bila shaka, pia Jonas atafurahi sana...Asante, rafiki yangu... Mamake Kassech atashangaa sana...Nitakupigia simu baadaye, kwaheri!

OUTRO:

Tunafikia mwisho wa sehemu ya saba ya hadithi yetu ya “Mwana Mpotevu- **Kisa cha kina mama wawaleao watoto wao bila baba zao barani Afrika**”. Aster amefanikiwa kumpata mtoto aliyekuwa ametoweka. Lakini mbona akashughulika kiasi hicho? Alikuwa na sababu nyingine? Hayo utayajua vizuri kwenye sehemu ijayo. Kumbuka, ukitaka kusikiliza sehemu hii tena, au kuwasilisha maoni na mapendekezo yako, fungua ukurasa wetu wa tovuti dw.de/lbe. Tukutane kwenye sehemu ijayo- kwaheri!